

Mwongozo wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea ni kazi inayoyatalii kwa uketo masuala muhimu ya kiuchambuzi kuhusu riwaya ya Ken Walibora iitwayo *Kidagaa Kimemwozea*. Mwongozo huu umebainisha maudhui, dhamira, migogoro, mbinu za uandishi na za lugha, pamoja na wahusika na uhusika wao katika matini chanzi. Mwongozo huu ni muhimu kwa mtahiniwa wa KCSE kwa namna unavyoviweka bayana na kwa njia sahili vipengele mbalimbali vya kiuchambuzi. Fauka ya hayo, *Mwongozo wa Kidagaa Kimemwozea* una tathmini ya kila sura punde baada ya mtiririko wake. Aidha kazi hii ina vielelezo vya maswali ya utahini yanayokusudia kumwanda mtahiniwa kwa kumpa uzoovu wa dhati na wa kutosha kwa mitihani ya riwaya husika. Ni matumaini yetu kuwa kazi hii kuntu itampa mwanafunzi mwelekeo bora na wa upesi kuhusu ujuzi na uelewa wake wa kushughulikia maswala na maswali ya riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.

P. I. Iribemwangi ni mwanaisimu, mwandishi, msomi na mwalimu mwenye tajriba pevu katika ufundishaji wa Kiswahili. Dkt. Iribemwangi ni Mhadhiri Mkuu wa isimu ya Kiswahili katika Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Pamoja na kazi yake ya uhadhiri, Dkt. Iribemwangi ni mtaalamu wa tafsiri na pia ni mchambuzi wa vitabu na maswala ya siasa katika vyombo mbalimbali vya habari. Vilevile, yeye ni mwandishi ambaye ameandika na kuhariri vitabu na makala zaidi ya arobaini. Dkt. Iribemwangi pia ni mtunzi wa bunilizi ambaye ameandika tamthilia na hadithi fupi nyingi.

Modgen Chisia ni mwalimu wa tajriba pevu katika kuwaandaa wanafunzi kwa somo la Kiswahili na Fasihi yake katika shule za upili. Amefundisha katika shule kadhaa jijini Nairobi zikiwemo Nairobi Muslim Academy, Shule ya Upili ya Sunshine na Light Academy. Ana shahada ya kwanza katika Elimu kutoka katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Aidha, Chisia ana Shahada ya Uzamili katika Kiswahili kutoka katika chuo kicho hicho. Kwa sasa anashughulikia kazi muhimu za shule ya upili, vyuo na vyuo vikuu ambazo zitachapishwa hivi karibuni.

MWONGOZO WA RIWAYA KIDAGAA YA KIMEMWOZEA

P. I. Iribemwangi
Modgen Chisia

